# HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

## MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI

## TAREHE 07.05.2021

**A. WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ibrahimu I. Chiputula | - | Diwani Kata ya Mpeta | – M/Kiti |
| 2. | Mhe. Anthony M. Chihako | - | Diwani Kata ya Msikisi | - M/M/Kiti |
| 3. | Mhe. Jafari M. Mkwanda | - | Diwani Kata ya Chiwata | -Mjumbe |
| 4. | Mhe. Fatuma H. Eriyo | - | Diwani Viti Maalum | “ |
| 5. | Mhe. Ajali M. Mpataga | - | Diwani Kata ya Lulindi | “ |
| 6. | Mhe. Samson E. Bushiri | - | Diwani Kata ya Mpindimbi | “ |
| 7. | Mhe. Hamza Kalembo | - | Diwani Kata ya Lukuledi | “ |
| 8. | Mhe. Yusuphu M. Chihakala | - | Diwani Kata ya Chiwale | “ |
| 9. | Mhe. Mwanaidi Stambuli | - | Diwani Viti Maalum | “ |
| 10. | Mhe. Mwanaidi Malambo | - | Diwani Viti Maalum | “ |
| 11. | Mhe. Stella L. Uchinga | - | Diwani Viti Maalum | “ |
| 12. | Mhe. Rashidi M. Njerero | - | Diwani Kata ya Sindano | “ |
| 13. | Mhe. Mohamed Mkokoto | - | Diwani Kata ya Namalenga | “ |
| 14. | Mhe. Ramadhani J. Chilumba | - | Diwani Kata ya Mnavira | “ |
| 15. | Mhe. Ismail Chilumba | - | Diwani Kata ya Chikundi | “ |
| 16. | Mhe. Jafari K. Mnandowe | - | Diwani Kata ya Mpanyani | “ |
| 17. | Mhe. Dominick G. Millanzi | - | Diwani Kata ya Mlingula | “ |
| 18. | Mhe. Mohamedi A. Chilumba | - | Diwani Kata ya Nangoo | " |
| 19. | Mhe. Edward E. Mahelela | - | Diwani Kata ya Chikoropola | ” |
| 20. | Mhe. Agnes Namwala | - | Diwani Kata ya Nanjota | ” |
| 21. | Mhe. Juma R. Polle | - | Diwani Kata ya Mijelejele | ” |
| 22. | Mhe. Kasembe J. Ponela | - | Diwani Kata ya Lipumburu | ” |
| 23. | Mhe. Arafat Kokocha | - | Diwani Kata ya Mbuyuni | ” |
| 24. | Mhe. Joyce Piteje | - | Diwani Viti Maalum | ” |
| 25. | Mhe. Greta Mrope | - | Diwani Viti Maalum | ” |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 26. | Mhe. Mussa A. Shabani | - | Diwani Kata ya Mchauru | ” |
| 27. | Mhe. Asina Lipopola | - | Diwani Viti Maalum | ” |
| 28. | Mhe. Stella M. Kambanga | - | Diwani Kata ya Ndanda | ” |
| 29. | Mhe. Hadija Mkanda | - | Diwani Viti Maalum | ” |
| 30. | Mhe. Mohamed Livate | - | Diwani Kata ya Chikukwe | ” |
| 31. | Mhe. Juma M. Satmah | - | Diwani Kata ya Chiungutwa | “ |
| 32. | Mhe. Suzana J. Achimpota | - | Diwani Viti Maalum | “ |
| 33. | Mhe. Yakobo S. Yakobo | - | Diwani Kata ya Namatutwe | “ |
| 34. | Mhe. Douglas D. Mkapa | - | Diwani Kata ya Lupaso | “ |
| 35. | Mhe. Amina Mpandula | - | Diwani Kata ya Chigugu | “ |
| 36. | Mhe. Asina Ngoma | - | Diwani Viti Maalumu | “ |
| 37. | Mhe. Hamisi LIngwelo | - | Diwani Kata ya Nanganga | “ |
| 38. | Mhe. Edith Chinguwile | - | Diwani Viti Maalum | “ |
| 39. | Mhe. Nestory Chilumba | - | Diwani Kata ya Mwena | “ |
| 40. | Mhe. Ahamadi K. Abedi | - | Diwani Kata ya Makong’onda | “ |
| 41. | Mhe. Faraji Y. Wadi | - | Diwani Kata ya Namajani | “ |
| 42. | Mhe. Wema D. Pokoho | - | Diwani Viti Maalum | “ |
| 43. | Mhe. Saimon D. Mpili | - | Diwani Kata ya Chikunja | “ |
| 44. | Mhe. Yusuph B. Mlaponi | - | Diwani Kata ya Namwanga | “ |

## B. WATENDAJI WALIOHUDHURIA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bibi. Changwa M. Mkwazu | - | Mkurugenzi Mtendaji (H/W) – Katibu |
| 2. | Bibi. Kulwa Maiga | - | Kaimu Afisa Mazingira (H/W) |
| 3. | Bw. Gift Mlay | - | Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii(H/W) |
| 4. | Bw. Deogratius M. Kaijage | - | Kaimu Mwanasheria (H/W) |
| 5. | Bw. Makarious Kakema | - | Mkaguzi wa Ndani (H/W) |
| 6. | Bw. Henry Mushi | - | Kaimu Afisa Manunuzi (H/W) |
| 7. | Bw. Thobias L. Mkude | - | Mratibu wa TASAF (H/W) |
| 8. | Bw. Anania Kamaghe | - | Kaimu Afisa Kilimo (H/W) |
| 9. | Bw. Gabriel K. Joshua | - | Afisa Ardhi na Maliasili (H/W) |
| 10. | Bw. Ally S. Nyambate | - | Afisa Elimu Sekondari (H/W) |
| 11. | Bw. Godfrey Y. Makenzi | - | Kaimu Afisa Mipango (H/W) |
| 12. | Bibi. Tatu L. Kazibure | - | Afisa Uchaguzi (H/W) |

13. Bw. Muksin K. Kilima - Kaimu Afisa Elimu Msingi (H/W)
14. Bw. Edward Msafiri - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (H/W)
15. Bw. Ally S. Mkungwa - Afisa Ardhi Mteule (H/W)
16. Bw. Anold R. Marandu - Kaimu Afisa TEHAMA (H/W)
17. Dr. Abdul Rashidi - Kaimu Mganga Mkuu (H/W)
18. Bw. Rustely E. Ndanzi - Afisa Nyuki (H/W)
19. Bw. Zedekia Mtawa - Kaimu Mweka Hazina (H/W)
20. Bw. Ryoba Magabe - Afisa Mifugo (H/W)
21. Bw. Nelson John - Kaimu Afisa Utumishi (H/W)

**C. WAGENI WAALIKWA**

1. Bibi Edith Shayo - Mwakilishi wa Katibu Tawala (M)
2. Bw. Mohamed Aziz Fakili - Katibu Tawala (W)
3. Bw. Fakili Nyakunga - DIO
4. Bw. Selemani Kambona - Mwakilishi RUWASA (H/W)
5. Bw. Mohamed Mwinyi - Ag. DSO
6. Capt. K.E. Masali - A/DET.COMD SINDANO
7. LT J.T Malakasuka - A/OC -07/691 Regt
8. Maj. JKJ Muhidini - Mshauri wa Jeshi la Akiba (W)
9. Bibi Ziada F. Mponela - Mwakilishi OCD
10. Bw. Chihongaki S.M - Kamanda TAKUKURU (W)
11. S/SI Ibrahim i. Badiri - Ag. DFO
12. Eng. William Tigahwa - Meneja TARURA (H/W)
13. Bw. John Kimario - Tech. TARURA (H/W)
14. Eng. Emmanuel James - TARURA (H/W)
15. Bw. Fikiri Lukanga - Ag. D/O Lisekese
16. Bw. Ali A. Kuchele - D/O Chiungutwa
17. Bw. Paulo Simwela - D/O Chikundi
18. Bibi Emmy R. Ng'ola - D/O Lulindi
19. Bw. Titho N. Stambuli - D/O Mchauru
20. Bibi Zainabu Chinowa - Katibu CCM (W)
21. Bibi Mwanahamisi Faki - Katibu UWT (W)
22. Bw. Leonard O. Undani - Mwenyekiti CHADEMA (W)

23. Bw. Dadi M. Dadi - Katibu CHADEMA (W)
24. Bw. Halinga Richard - Mtendaji kata Chikundi
25. Bw. Rahim Seleman - Mtendaji kata Nanjota

**D. SEKRETARIETI**

1. Bw. Wallace Makunda - Mwandishi wa mikutano (H/W)
2. Bw. Mwachura Innocent - Mwandishi wa mikutano (H/W)

**MUHT. NA. MDC 2020/2021: KUFUNGUA MKUTANO**

Mara baada ya Mwenyekiti wa Halmashauri, Makamu Mwenyekiti na Katibu kuingia ukumbini, wimbo wa Taifa uliimbwa kisha Mwenyekiti wa Halmashauri alisoma Sala ya Halmashauri.

Baada ya Mwenyekiti kumaliza kusoma Sala ya Halmashauri aliwakaribisha wajumbe, wageni waalikwa, watendaji na wadau wengine wote waliohudhuria katika Mkutano huo wa kawaida wa baraza la Madiwani, aliwaomba wajumbe wazingatie kuunda katika kuendesha mkutano huo aidha alitoa taarifa kwamba kufuatia kifo cha Mheshimiwa Shaibu Mpochi (Diwani kata ya Mitesa) ambae alikuwa mjumbe wa ALAT Mkoa, nafasi hiyo itajazwa na **Mhe. Kasembe Ponela (Diwani kata ya Lipumburu).**

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi alifungua mkutano huo mnamo saa 4.51 asubuhi.

**MUHT. NA. MDC 2020/2021: KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda zifuatazo ziliwasilishwa na kujadiliwa katika mkutano huo

1. Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha agenda
3. Maswali ya papo kwa papo
4. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano wa tarehe 29. 01.2021
5. Yatokanayo na muhtasari wa mkutano wa tarehe 29/01/2021.
6. Kujibu hoja mbalimbali zilizopokelewa kutoka kwa waheshimiwa Madiwani.
7. Kupokea na kujadili taarifa za kamati za kudumu za Halmashauri.
   - (i) Kamati ya Kudhibiti UKIMWI
   - (ii) Kamati ya Elimu, Afya na Maji
   - (iii) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira

(iv) Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango

8. Nasaha za viongozi
9. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
10. Kufunga Mkutano

**MUHT. NA. MDC 2020/2021: MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kwamba amepokea majina ya wajumbe wanne ambao wameomba kuuliza maswali ya papo kwa papo aliwataja wajumbe hao kuwa ni:-

1. Mhe. Hamisi T. Ling'welo **(Diwani Kata ya Nanganga)**
2. Mhe. Douglas D. Mkapa **(Diwani Kata ya Lupaso)**
3. Mhe. Kasembe Ponela **(Diwani Kata ya Lipumburu)**
4. Mhe. Juma R. Polle **(Diwani Kata ya Mijelejele)**

Aliwakaribisha wajumbe hao ili waulize maswali.

1. **Mhe. Hamisi T. Ling'welo (Diwani Kata ya Nanganga)** alitaka kufahamu kanuni gani zinazotumika ili kupata chama kingine cha Ushirika (AMCOS) pia alitaka kujua kama kila kijiji kinaweza kuwa na chama chake cha Ushirika.

**Ufafanuzi:-**
Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (H/W) alianza kwa kueleza kuwa Ushirika ni umoja wa hiari ambapo uanzishwaji wake huwa ni kwa lengo la kujikwamua kiuchumi.

Alisema kigezo kikubwa ambapo hutumika kutoa idhini ya kuanzisha ushirika ni pale itakapothibitisha kuwa wahusika walioomba kuazisha ushirika katika eneo Fulani, eneo hilo linaweza kuzalisha tani 700.

Kuhusu kila kijiji kuwa na chama chake cha ushirika, alieleza kwamba kigezo kikubwa kinachozingatiwa ni kama alivyoainisha awali kwa maeneo husika kuweza kuzalisha tani zisizopungua 700.

2. **Mhe. Douglas D. Mkapa (Diwani Kata ya Lupaso)** alitaka kujua Serikali ina mpango gani kutoa huduma bure kwa wagonjwa wa moyo (BP) kwani kufuatia mabadiliko ya mitindo ya maisha imepelekea kuwepo kwa wagonjwa wengi wenye ugonjwa huo na kutokana na kuwa na kipato duni inafanya washindwe kumudu gharama za matibabu.

**Ufafanuzi:-**
Kaimu Mganga Mkuu (H/W) aliwaeleza wajumbe kwamba Sera ya utoaji wa huduma ya afya imeweka utaratibu katika kutoa misamaha kwa baadhi ya magonjwa ya kudumu ili kuwasaidia wagonjwa wenye magonjwa kupata huduma bure, aliongeza kuwa ni vyema wagonjwa wenye changamoto hizo wafuate taratibu zilizopo ili kuweza kupata misamaha hiyo.

3. **Mhe. Kasembe Ponela (Diwani Kata ya Lipumburu)** alitaka kujua Halmashauri ina mpango gani wa kuisaidia zahanati ya Njawara ili kuwezesha kukamilisha ujenzi wake.

**Ufafanuzi:-**
Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa, miradi ya maendeleo itaendelea kupatiwa fedha kwa kuzingatia hali ya makusanyo itakavyokuwa nzuri, na kuhusu zahanati ya Njawara alimuomba mjumbe mtoa hoja avute subira ili kupata uhakika kuhusu chanzo kilichopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

4. **Mhe. Juma R. Polle (Diwani Kata ya Mijelejele)** alianza kwa kueleza kuwa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na kuwa na jukumu la kusimamia hali ya usalama wan chi, pia vinazalisha mali mbalimbali, alitoa mfano Jeshi la Magereza ambayo kwa sasa inatengeneza chaki zinazotumika shuleni.

Alishauri kupitia fursa hiyo Halmashauri ione umuhimu wa kushirikiana na Jeshi hilo ili kuweza kupata bidhaa hiyo ambayo kwa kiasi kuikubwa itasaidia katika shule zetu.

Katibu alimshukuru mjumbe kwa ushauri huo na kueleza kuwa utafanyiwa kazi.

**MUHT. NA. MDC 2020/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA TAREHE 29/01/2021**

Muhtasari uliwasilishwa na wajumbe waliupokea.

Masahihisho yalifanyika katika ukurasa wa 2 jina namba 25, “**Mhe. Joyce Pileje**” lisomeke “**Mhe. Joyce Piteje**”.
Katika ukurasa wa 8 mstari wa 21 neno “**imewasilishwwa**” lisomeke “**imewasilishwa**”
Katika ukurasa wa 11 mstari wa 10 neno “**lililopopo**” lisomeke “**lililopo**”
Katika ukurasa wa 19 mstari wa 25 neno “**Lipaso**” lisomeke “**Lupaso**”.

Baada ya masahihisho hayo, Mwenyekiti na Katibu waliweka saini zao kuthibitisha kuwa ni kumbukumbu halali ya mkutano huo.

**MUHT. NA. MDC 2020/2021: YATOKANAYO NA MUHTASARI HUO**

| KUTOKA MUHT. NA | AZIMIO | MTEKELEZAJI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| | 1. Watendaji kutoka taasisi za TARURA na RUWASA waalikwe katika mikutano ya baraza la Madiwani pamoja na vikao vya kamati za kudumu ili kutoa ufafanuzi | **DED** | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kuhusu hoja za maji na barabara. | | |
| | 2. Jitihada za makusudi zifanyike ili hadi kufikia tarehe 31/03/2021, mradi wa maji Chipingo na Mkaliwata uanze kutoa huduma kwa wananchi. | **Meneja RUWASA** | |
| | 3. Wajumbe walikubaliana na pendekezo la wajumbe wa kamati ya Fedha, Utawala na Mipango (FUM) kufanya ziara ya tathmini katika vyanzo vya mapato ya Halmashauri kwa lengo la kupata uzoefu wa namna mapato hayo yanavyokusanywa pamoja na kuhakiki mapato hayo. | **DED** | |

Kutoka azimio namba 3, **Mhe. Douglas D. Mkapa (Diwani Kata ya Lupaso)** alisema ilikuwa ni vyema wajumbe wa baraza la Madiwani wapewe angalau taarifa fupi kuhusiana na mafanikio na changamoto ya zoezi la tathmini ya vyanzo vya mapato lililofanywa na wajumbe wa kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.

**Ufafanuzi:-**

Mwenyekiti (H/W) alisema kupitia zoezi hilo kamati pia iliweza kukusanya mapato na aliwaomba wajumbe pindi watakapojadili taarifa za kamati za kudumu, ndio eneo sahihi ambapo wanaweza kuona maoni mbalimbali yaliyotolewa na wajumbe wa kamati ya Fedha, Utawala na Mipango baada ya kukamilisha zoezi hilo, aliongeza manoni hayo yalilenga kuongeza hali ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri.

Wajumbe walikubaliana na utekelezaji wa maazimio hayo.

**MUHT. NA. MDC 2020/2021 : KUJIBU HOJA MBALIMBALI ZILIZOPOKELEWA KUTOKA KWA WAHESHIMIWA MADIWANI**

Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa hajapokea hoja yoyote kutoka kwao.

**MUHT. NA. MDC 2020/2021 : KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU**

**1. KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI**

Mwenyekiti wa kamati ya Kudhibiti UKIMWI **Mhe. Antony M. Chihako (Diwani Kata ya Msikisi)** aliwasilisha taarifa ya kamati ya Kudhibiti UKIMWI na aliungwa mkono na wajumbe wa kamati hiyo.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Anthony M. Chihako | Diwani Kata ya Msikisi |
| 2. | Mhe. Ibrahim I. Chiputula | Diwani Kata ya Mpeta |
| 3. | Mhe. Wema B. Pokoho | Diwani Viti Maalum |
| 4. | Mhe. Juma M. Satmah | Diwani Kata ya Chiungutwa |
| 5. | Mhe. Selemani Yakobo | Diwani Kata ya Namatutwe |
| 6. | Mhe. Suzana J. Achimpota | Diwani Viti Maalum |
| 7. | Mhe. Nestory G. Chilumba | Diwani Kata ya Mwena |

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:-

**Mhe. Ramadhani J. Chilumba (Diwani Kata ya Mnavira)** alisema katika zahanati ya Mnavira kuna upungufu wa watumishi hali inayopelekea watoa huduma katika kituo cha CTC kutumika kutoa huduma za uzazi kwa akina mama wajawazito alitaka kujua kama jambo hilo ni sahihi.

**Ufafanuzi:-**

Kaimu Mganga Mkuu (H/W) aliwaeleza wajumbe kuwa suala hilo haliko sawa kwa kuwa, watumishi wanaotakiwa kutoa huduma za uzazi kwa akina mama wajawazito wanapaswa kuwa na weledi wa jambo hilo.

Aliahidi kulifuatilia suala hilo Katibu aliwakumbusha wajumbe kuwa pindi wanapoona mambo hayako sawa katika maeneo yao wasisubiri vikao, aliwaomba watoe taarifa mapema ili hatua ziweze kuchukuliwa.

**Mhe. Abdallah S. Abdallah (Diwani Kata ya Mkululu)** alitaka kujua hali ya maambukizi ya UKIMWI ikoje, pia aliongeza kuwa kumekuwa na changamoto kwa WAVIU kutembea mwendo mrefu kwa ajili ya kupata huduma, alitaka kujua kama hakuna mpango wowote wa kuwasogezea huduma karibu.

**Ufafanuzi:-**

Kaimu Mganga Mkuu (H/W) aliwaeleza wajumbe kuwa hali ya maambukizi imefikia asilimia 2.2, kwa upande wa upatikanaji wa huduma za afya kwa WAVIU alieleza kuwa zahanati zote na vituo vya afya vinavtoa huduma hizo.

**Mhe. Juma M. Satmah (Diwani Kata ya Chiungutwa)** aliwaeleza wajumbe kuwa kutokana na utaratibu wa uwasilishaji wa taarifa za kamati katika mkutano wa baraza la Madiwani ni vyema wajumbe wajikite zaidi katika mapendekezo yaliyotolewa na kamati husika.

Wajumbe walikubaliana na ushauri uliotolewa na baada ya majadiliano ya kina katika taarifa ya kamati ya kudhibiti UKIMWI waliazimia kama ifuatavyo:-

**Azimio:-**

1. Mganga Mkuu (H/W) aende katika zahanati ya Mnavira ili kushughulikia changamoto iliyojitokeza kwa wajumbe wa CTC kutumika kutoa huduma ya uzazi katika zahanati hiyo.

**2. KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI**

Mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Afya na Maji **Mhe. Ajali M. Mpataga (Diwani Kata ya Lulindi)** aliwasilisha kwa wajumbe taarifa ya kamati hiyo na aliungwa mkono na wajumbe wa kamati hiyo.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Edward E. Mahelela | - | Diwani Kata ya Chikoropola |
| 2. | Mhe. Juma M. Satmah | - | Diwani Kata ya Chiungutwa |
| 3. | Mhe. Edwin S. Kasembe | - | Diwani Kata ya Namwanga |
| 4. | Mhe. Asha M. Akida | - | Diwani Viti Maalum |
| 5. | Mhe. Omari Mkoko | - | Diwani Kata ya Chikunja |
| 6. | Mhe. Geofrey B. Alimwike | - | Diwani Kata ya Chiwata |
| 7. | Mhe. Onesmo L. Millanzi | - | Diwani Kata ya Chikukwe |
| 8. | Mhe. Asina S. Lipopola | - | Diwani Viti Maalum |
| 9. | Mhe. Leodgar I. Chilala | - | Diwani Kata ya Mpanyani |
| 10. | Mhe. Musa M. Mbweso | - | Diwani Kata ya Mitesa |
| 11. | Mhe. Mwanaidi H. Malambo | - | Diwani Viti Maalum |
| 12. | Mhe. Douglas D. Mkapa | - | Diwani Kata ya Lupaso |
| 13. | Mhe. Ramadhani J. Chilumba | - | Diwani Kata ya Mnavira |
| 14. | Mhe. Cornelio D. Mummelele | - | Diwani Kata ya Sindano |
| 15. | Mhe. Ester T. Ng'itu | - | Diwani Viti Maalum |

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:-

**Majadiliano:-**

**Mhe. Juma R. Polle (Diwani Kata ya Mijelejele)** alitaka kupata ukweli kuhusiana na taarifa ya kuhamishwa kwa shule Maalum Lulindi.

Mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Afya na Maji aliunga mkono hoja hiyo na kueleza kuwa wakazi wa Lulindi wanawasiwasi mkubwa kufuatia kuwepo kwa taarifa hiyo, alishauri

kupitia mkutano huo wa baraza la Madiwani ni vyema taarifa kamili ya suala hilo ingetolewa.

Pia aliongeza kuwa kuna fedha Tsh. 80,000,000/= zimeingia katika akaunti ya Shule hiyo lakini zimeezuliwa kutumika jambo ambalo linaongeza sintofahamu katika jambo hilo.

**Ufafanuzi:-**
Katibu alisema ni kweli kuna maelekezo yametolewa kuhusiana na shule hiyo, aliongeza kuwa yeye binafsi hajapokea maelekezo yoyote kuhusiana na kuhamisha shule hiyo.

Kuhusu fedha Tsh. 80,000,000/= zilizopokelewa katika shule hiyo, alikiri kuwa alipokea maelekezo kuwa fedha hizo zisitumike hadi pale maelekezo mengine yatakapotolewa.

**Mhe. Juma M. Satmah (Diwani Kata ya Chiungutwa)** alisema kimsingi anakubaliana na maelezo yaliyotolewa na Katibu kuhusu hoja hiyo ingawa aliongeza kuwa katika mojawapo ya mkutano wa baraza la Madiwani wajumbe waliazimia kuwa shule hiyo isihamishwe na kupelekwa eneo linguine, aliongeza kuwa suala hilo lisipofanyika kwa uangalifu linaweza kusababisha misuguano isiyo ya lazima.

Aliongeza kuwa inasemekana shule hiyo itahamia kwa kutokana na ukosefu wa eneo. Alishauri kama sababu itakuwa hiyo ni vyema wananchi wa Lulindi wapewe nafasi ya kutoa eneo ili shule hiyo isihamishwe kutoka eneo hilo.

Mwenyekiti (H/W) alikubaliana na maelezo ya mjumbe aliyepita na kuongeza kuwa huo ubakie kama ushauri wa wajumbe wa baraza la Madiwani katika hoja hiyo.

**Mhe. Juma R. Polle (Diwani Kata ya Mijelejele)** alisema kuna taarifa ambazo zinaendelea kusambaa kuhusiana na ujenzi wa shule mbili mpya za Sekondari ambayo shule moja itajengwa katika Kata ya Chikunja aliomba kupata ufafanuzi wa suala hilo.

**Ufafanuzi:-**
Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Afya na Maji alisema jambo hilo halijawahi kuwasilishwa katika kamati ya Elimu, Afya na Maji , aidha aliwakumbusha wajumbe kuwa wao ndio wanapaswa kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu ustawi wa Halmashauri.

**Mhe. Douglas D. Mkapa (Diwani Kata ya Lupaso)** alikubaliana na maelezo ya Mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Afya na Maji na kueleza kuwa yeye kama mjumbe wa kamati hiyo, kamati hiyo haijawahi kujadili suala hilo katika vikao vyake.

Aliongeza kuwa endapo itatokea basi anaamini hoja hiyo itawasilishwa katika kamati hiyo ili wajumbe waweze kutoa maoni yao.

Mwanasheria (H/W) aliwaomba wajumbe wazingatie taratibu kwa kujadili taarifa ambazo zipo katika kabrasha, pia aliwasihi wakubaliane na maelezo yaliyotolewa na Katibu.

Mjumbe mtoa hoja alisema bahati mbaya hapo awali kumewahi kutokea taarifa kama hizo ambazo hazikuwa rasmi lakini mwisho wake zimekuwa taarifa za kweli, alitoa rai kuwa ni vyema tusirejee katika makosa hayo.

**Ushauri:-**
Afisa Serikali za Mitaa (M) aliwashauri wajumbe kuwa ni vyema wawe na subira katika kulishughulikia kuhusu kuunda tume ya kufuatilia suala hilo Mamlaka za juu, alishauri kabla ya kwenda katika Mamlaka za juu ni vyema suala hilo liwasilishwe katika ngazi ya Mkoa.

Aliahidi kulichukua suala hilo kwa hatua zaidi.

Mwenyekiti (H/W) aliwasihi wajumbe wakubaliane na ushauri uliotolewa na Afisa Serikali za Mitaa (M).

**Mhe. Edward E. Mahelela (Diwani Kata ya Chikoropola)** alisema katika zahanati ya Mapili kuna Mtumishi mmoja tu hali inayopelekea mtumishi huyo kuelemewa na majukumu, vilevile alisema bado kuna sintofahamu ya mradi wa maji Chipingo – Mkaliwata.

**Ufafanuzi:-**
Kaimu Mganga Mkuu (H/W) alikiri kuwepo kwa upungufu wa watumishi wa afya katika maeneo mbalimbali ikiwemo zahanati ya Mapili, aliongeza kuwa tayari Idara imepokea mtumishi mmoja ambae atapelekwa katika zahanati hiyo.

Kuhusu suala la mradi wa maji wa Chipingo – Mkaliwata, Mwenyekiti alimkaribisha mwakilishi kutoka RUWASA (H/W) ili aweze kutoa ufafanuzi.

Mwakilishi kutoka RUWASA alisema changamoto iliyopo katika mradi huo ni kupasuka kwa mabomba mara kwa mara hali inayofanya mradi kutokukamilika kwa wakati.

**Mhe. Abdallah S. Abdallah (Diwani kata ya Mkululu)** alisema tatizo la kupasuka kwa mabomba lipo katika karibu miradi yote ya maji, hali inayofanya miradi hiyo kutokukamilika na kushindwa kutoa huduma kwa wananchi.

Katibu alikubaliana na uwepo wa changamoto nyingi katika utekelezaji wa miradi ya maji, alisema mojawapo ya changamoto ilifanywa na msanifu wa miradi hiyo jambo ambalo limesababisha marekebisho mbalimbali kufanyika katika miradi hiyo ikiwemo ubadilishaji wa mabomba.

**Mhe. Samson E. Bushiri (Diwani kata ya Mpindimbi)** alisema anakubaliana na maelezo yaliyotolewa na Katibu lakini hajaridhishwa na maji yaliyotolewa na mwakilishi wa RUWASA. Aliongeza kuwa kuna urasimu mkubwa katika kutekeleza miradi hiyo.

Alishauri ni vyema RUWASA waeleze lini miradi hiyo itakamilika ili iweze kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

**Ufafanuzi:-**
Mwakilishi wa RUWASA alisema mradi wa Chipingo – Mkaliwata upo katika majaribio ambapo mapungufu yanayojitokeza yanafanyiwa marekebisho.

**Mhe. Edward E. Mahelela (Diwani kata ya Chikoropola)** alisema kwa kuwa mradi huo unatekelezwa katika eneo lake, ambapo kupitia kikao cha pamoja kati ya wananchi na wataalam kutoka Mkoani, walielezwa kuhusiana na utekelezaji wa mradi huo.

Alishauri kufuatia changamoto zilizopo vyema RUWASA warudi tena kwa wananchi na kuwaeleza kinachoendelea katika utekelezaji wa mradi huo.

**Ushauri:-**
**Mhe. Douglas D. Mkapa (Diwani kata ya Lupaso)** alishauri ili kuliweka sawa jambo hilo ni vyema mawasiliano yafanyike na Meneja wa RUWASA (H/W) ili kupata taarifa kamili kuhusiana na ukamilishaji wa miradi ya maji.

Wajumbe walikubaliana na taarifa hiyo. Mwenyekiti wa kamati ya Elimu, Afya na Maji, aliwashukuru wajumbe kwa jinsi walivyoijadili taarifa ya kamati hiyo. Aidha aliwakumbusha wajumbe suala zima la kusimamia kikamilifu maazimio yote yaliyotolewa katika mkutano wa wadau wa elimu kwa lengo la kuinua hali ya ufaulu katika shule zetu. Vilevile aliongeza kuwa kupitia Mfuko wa elimu, shule nyingi zimepewa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu ya shule. Aliwaomba wajumbe wasimamie kikamilifu utekelezaji wa miradi hiyo katika maeneo hayo.

**Azimio:**

1. Mawasiliano yafanyike na Meneja wa RUWASA (H/W) ili kupata taarifa kamili kuhusiana na ukamilishaji wa miradi ya maji.

**KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA**

**Mhe. Juma R. Polle (Diwani kata ya Mijelejele)** kwa niaba ya **Mhe. Jaffari M. Mkwanda (Diwani kata ya Chiwata na Mwenyekiti wa kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira)** aliwasilisha taarifa ya kamati hiyo kwa wajumbe na aliungwa mkono na wajumbe wa kamati hiyo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. | Jafari M. Mkwanda | - | Diwani Kata ya Chiwata |
| 2. | Mhe. | Ibrahim I. Chiputula | - | Diwani Kata ya Mpeta |
| 3. | Mhe. | Asina S. Lipopola | - | Diwani Viti Maalum |
| 4. | Mhe. | Kokocha M. Arafati | - | Diwani Kata ya Mbuyuni |
| 5. | Mhe. | Juma R. Polle | - | Diwani Kata ya Mijelejele |
| 6. | Mhe. | Joyce G. Piteje | - | Diwani Viti Maalum |
| 7. | Mhe. | Greta R. Mrope | - | Diwani Viti Maalum |
| 8. | Mhe. | Agnes P. Namwala | - | Diwani Kata ya Nanjota |
| 9. | Mhe. | Hadija S. Mkanda | - | Diwani Viti Maalum |
| 10. | Mhe. | Stella M. Kambanga | - | Diwani Kata ya Ndanda |
| 11. | Mhe. | Mussa A. Shabani | - | Diwani Kata ya Mchauru |
| 12. | Mhe. | Mohamed A. Chilumba | - | Diwani Kata ya Nangoo |
| 13. | Mhe. | Kasembe J. Ponela | - | Diwani Kata ya Lipumburu |
| 14. | Mhe. | Mohamed H. Livate | - | Diwani Kata ya Chikukwe |
| 15. | Mhe. | Edward E. Mahelela | - | Diwani Kata ya Chikoropola |
| 16. | Mhe. | Hamisi T. Ling'welo | - | Diwani Kata ya Nanganga |
| 17. | Mhe. | Amina S. Mpandula | - | Diwani Kata ya Chigugu |

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:-

**Majadiliano:-**
**Mhe. Samson E. Bushiri (Diwani kata ya Mpindimbi)** alitaka kujua nini kinachosababisha miradi ya umeme wa REA kuchukua muda mrefu kukamilika.

Vilevile alihoji kuhusiana na mpango wa Serikali wa kutoa pembejeo za zao la korosho kwa wakulima, halafu kuwakata Sh. 110/= kwa kila kilo bila ya kujali kama mkulima husika alipata na hakupata pembejeo hizo.

**Ufafanuzi:-**

**Mhe. Juma R. Polle (Diwani kata ya Mijelejele)** alieleza kuwa hoja ya maeneo mengi kutounganishwa na umeme wa REA, yeye binafsi aliwasiliana na Meneja wa TANESCO ambae alieleza kuwa wananchi waendelee kuvuta subira kwa kuwa bado mpango huo unaendelea.

Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (H/W) alieleza kuwa suala la utaratibu wa upatikanaji na pembejeo za zao la korosho bado halijawa rasmi kwa kuwa bado vikao vinaendelea ili kupitia utaratibu mzima wa upatikanaji wa pembejeo hizo. Aliongeza kuwa kutakuwa na kikao kitakachofanyika Mtwara tarehe 10-11/5/2021 ili kujadili suala hilo.

**Mhe. Samson E. Bushiri (Diwani kata ya Mpindimbi)** alisema wazo la Serikali ni zuri lakini kuna haja ya kufanya tathmini katika suala hilo vilevile wakulima wapewe elimu ya kutosha ili kutoingia katika migogoro isiyo ya lazima.

**Mhe. Abdallah S. Abdallah (Diwani kata ya Mkululu)** alisema ni vyema Serikali ipate ushauri katika suala hilo, kwa kuwa kuna baadhi ya wakulima walishanunua wenyewe pembejeo kwa ajili ya mashamba yao na utaratibu unaelekeza kuwa kila kilo ya korosho itakayoingia ghalani itakatwa Shs. 110/=.

Aliongeza kuwa ni vyema na suala hilo liwe kwa wazi kama makato watakayokatwa yatakuwa mtaji kwa mwaka unaofuata.

**Mhe. Edward E. Mahelela (Diwani kata ya Chikoropola)** alisema hapo awali kuliwepo na mfuko wa pembejeo ambapo wakulima walikuwa wanakatwa kulingana na pembejeo walizochukua.

Alishauri suala hilo lishughulikiwe kwa umakini mkubwa kwani halijakaa vizuri.

**Azimio:-**

1. Halmashauri iendelee kufuatilia taarifa kuhusu utaratibu mpya wa upatikanaji wa pembejeo wa zao la korosho.

**Mhe. Juma M. Satmah (Diwani kata ya Chiungutwa)** alishauri Idara ya Kilimo, iendelee kulifuatilia kwa karibu suala hilo ili kupata usahihi wake na pindi litakapokamilika wajumbe wapewe taarifa.

**Mhe. Douglas D. Mkapa (Diwani kata ya Lupaso)** alitaka kujua lini barabara ya Umati – Mitonji itafunguliwa kwani wananchi walishafanya shughuli mbalimbali katika

maandalizi ya barabara hiyo na vilevile barabara hiyo ilishatengewa Sh. 12,000,000/= katika bajeti.

Vilevile Mwenyekiti (H/W) aliongeza kuwa kuna shida katika barabara ya Chikukwe – Napata ambayo haipitiki, alimuomba Meneja wa TARURA (H/W) atoe ufafanuzi kuhusu hoja hizo.

**Ufafanuzi:-**
Meneja TARURA (H/W) aliwaeleza wajumbe kwamba TARURA ilipata nafasi ya kuiona barabara ya Chikukwe – Napata ambayo inapitika.

Kuhusu kufungua barabara ya Umati – Mitonji, Meneja wa TARURA (H/W) alisema TARURA wanatekeleza barabara zipo katika mpango, lakini kwa barabara mpya kama ya Umati – Mitonji, utaratibu unaelekeza kwamba ili barabara kama hizo ziweze kufanyiwa kazi inabidi Halmashauri ipeleke fedha za kutengeneza barabara hizo TARURA ili ziweze kutekelezwe.

Mwenyekiti (H/W) alisema kwa namna maelezo yalivyotolewa ni vyema barabara hiyo ikawekwa katika bajeti ya mwaka 2022/2023 ili ipate fedha za kuweza kuitengeneza.

**Mhe. Yusuph Mlaponi (Diwani kata ya Namwanga)** alitaka kupata ufafanuzi kuhusu hatua iliyochukuliwa na Chama cha Ushirika cha Idannole kukopa fedha benki kwa ajili ya kuwalipa wakulima 16 wanaokidai chama hicho.

**Ufafanuzi:-**
Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (H/W) alisema kimsingi chama hicho bado ni kidogo na kutokana na matatizo yaliyokikumba chama hicho ndipo waliporidhia kukopa benki ili kuweza kuwalipa wakulima hao waliokuwa wanakidai chama hicho.

Mwenyekiti alihoji kama korosho za wakulima hao ziliuzwa, fedha zilienda wapi.

**Ufafanuzi:-**
Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (H/W) alisema kiuhalisia hoja hiyo imetokana na ubadhirifu na vilevile kutokana na chama hicho kushindwa kujiendesha.

**Mhe. Edward E. Mahelela (Diwani kata ya Chikoropola)** aliongeza kuwa tatizo lililopo ni kwamba hata Sheria za ushirika haziko wazi katika hoja kama hiyo hali ambayo inafanya kuwepo ugumu katika utekelezaji wake.

**Mhe. Faraji Y. Wadi (Diwani kata ya Namajani)** alitaka kujua kuhusu utatuzi wa mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Namaji na gereza la Namajani – Nawaje ipo katika hali gani.

**Ufafanuzi:-**
Meneja TARURA (H/W) alisema barabara ya Namajani – Nawaje inahudumiwa na TARURA (H/W) Masasi ambapo tayari Mkandarasi amechonga karibu kilometa 7.

Katibu alitoa ufafanuzi kuhusu mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na gereza la Namajani kuwa unaendelea kushughulikiwa ambapo taarifa zimeshafika makao makuu ya Jeshi la Magereza kwa ajili ya utekelezaji.

Wajumbe walikubaliana na taarifa hiyo pamoja na majadiliano yaliyojitokeza.

**KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO**

**Mhe. Anthony M. Chihako (Diwani Kata ya Msikisi)** kwa niaba ya Mwenyekiti wa Halmashauri **Mhe. Ibrahimu I. Chiputula** aliwasilisha katika mkutano taarifa ya kamati ya Fedha, Utawala na Mipango na aliungwa mkono na wajumbe wa kamati hiyo.

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ibrahimu I. Chiputula | Diwani Kata ya Mpeta |
| 2. | Mhe. Anthony M. Chihako | Diwani Kata ya Msikisi |
| 3. | Mhe. Jafari M. Mkwanda | Diwani Kata ya Chiwata |
| 4. | Mhe. Fatuma H. Eriyo | Diwani Viti Maalum |
| 5. | Mhe. Mhe. Ajali Mpataga | Diwani Kata ya Lulindi |
| 6. | Mhe. Samson E. Bushiri | Diwani Kata ya Mpindimbi |
| 7. | Mhe. Mwanaidi Stambuli | Diwani Viti Maalum |
| 8. | Mhe. Hamza S. Kalembo | Diwani Kata ya Lukuledi |
| 9. | Mhe. Ahamadi K. Abedi | Diwani Kata ya Makong'onda |
| 10. | Mhe. Yusuph M. Chihakala | Diwani Kata ya Chiwale |
| 11. | Mhe. Cecil D. Mwambe | Mbunge Jimbo la Ndanda |
| 12. | Mhe. Issa A. Mchungahela | Mbunge Jimbo la Lulindi |

Wajumbe waliipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:-

**Majadiliano:-**
**Mhe. Edward E. Mahelela (Diwani kata ya Chikoropola)** alisema kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ndiyo inayosimamia mapato na matumizi ya Halmashauri, alishauri kuona uwezekanao wa taarifa ya makusanyo ya mapato na matumizi ziwe

zinawasilishwa katika mikutano ya mabaraza ya Madiwani ili wajumbe wote wawe na uelewa wa makusanyo ya Halmashauri.

**Ufafanuzi:-**
Mwenyekiti (H/W) alisema kimsingi utaratibu unaotumika sasa katika kuwasilisha taarifa katika mkutano wa baraza la Madiwani ulipitishwa na baraza, aliongeza kuwa bado nafasi ipo kwa kupitia majadiliano ili kuweza kupata namna bora ya uwasilishaji wa taarifa hizo.

**Mhe. Jafari K. Mnandowe (Diwani kata ya Mpanyani)** alianza kwa kutoa pongezi kwa kamati ya Fedha kwa jinsi inavyotekeleza majukumu mbalimbali, alieleza kuwa kufuatia kuanzishwa kwa stendi ya Ndanda kumepelekea stendi nyingine kama vile stendi ya Madeco kufungwa jambo ambalo limeleta kero kubwa kwa wagonjwa wanaoenda kupata huduma za afya katika hospitali ya Ndanda.

**Mhe. Stella M. Kambanga (Diwani kata ya Ndanda)** aliunga mkono hoja ya mjumbe aliyepita na alihoji lini suala la stendi ya Ndanda litapatiwa ufumbuzi kwani bado kuna sintofahamu katika utekelezaji wake.

**Ufafanuzi:-**
Mwenyekiti (H/W) aliwaeleza wajumbe kuwa haoni kama ni busara kulijadili suala hilo, aliongeza kuwa kwa kuzingatia maslahi ya Halmashauri hoja hiyo inapaswa kuangaliwa kwa mapana zaidi, aidha aliendelea kueleza kwamba utekelezaji wa hoja hiyo unahusisha pia vyombo vya ulinzi na usalama, aliwaomba wajumbe hoja hiyo isijadiliwe katika mkutano huo bali isubiri vikao vingine.

**Mhe. Ramadhani J. Chilumba (Diwani kata ya Mnavira)** alitaka kujua Halmashauri ina mikakati gani kuhakikisha inadhibiti utoroshwaji wa Choroko kutoka maeneo ya Halmashauri ya Wilaya na kuingizwa Halmashauri ya Mji.

**Ufafanuzi:-**
Mwenyekiti (H/W) aliwaeleza wajumbe kuwa tayari kamati ya mapato ya (H/W) imeshaingiwa kusimamia suala hilo.

Vilevile aliongeza kuwa pamoja na kamati ya mapato kuagizwa kusimamia suala hilo, inapaswa kupewa ushirikiano mkubwa kutoka maeneo ya vijiji na kata kwani mazao hao yanatoka maeneo hayo na kuingizwa Halmashauri ya Mji, alisisitiza kila mtu kwa nafasi yake ashiriki kudhibiti hali hiyo na alikumbusha kuwa suala la udhibiti wa mapato ni jukumu la kila mtu.

Wajumbe walikubaliana na taarifa hiyo.

**MUHT. NA.MDC 2020/2021: NASAHA ZA VIONGOZI**

Mwenyekiti aliwakaribisha viongozi waliohudhuria katika mkutano huo ili watoe nasaha zao.

1. **Bibi Edith Shayo (Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa)** alianza kwa kutoa pole kufuatia misiba iliyoikumba Halmashauri na kupelekea kuwapoteza wenzetu, aliziombea roho za marehemu hao zipumzike mahali pema peponi.

   Baada ya salamu hizo za pole, aliwapongeza wajumbe, wageni waalikwa, watendaji na wakuu wengine wote kwa namna walivyoshiriki kikamilifu katika mkutano huo.

   Aliwakumbusha wajumbe kuzingatia sharia kanuni na taratibu katika suala zima la uendeshaji wa mikutano ya mabaraza ya Madiwani na aliwashauri wasisubiri vikao ndio wawasilishe hoja mbalimbali. Aliwakumbusha kuwa zinapojitokeza hoja mbalimbali waziwasilishe mapema ili ziweze kushughulikiwa.

   Alitoa rai kwa watendaji kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kikamilifu na kuhakikisha maagizo yote yanayotolewa yanatekelezwa kikamilifu na kwa wakati.

2. **Bw. Leonard O. Undani (Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo – CHADEMA (W)** alianza kwa kutoa pongezi namna ambavyo baraza la Madiwani linavyotekeleza kikamilifu majukumu yake.

   Aligusia kuhusiana na suala la upatikanaji wa pembejeo za zao la korosho na kueleza kuwa kuna kila sababu ya kuangalia kwa umakini mkubwa suala la utaratibu wa upatikanaji wa pembejeo hizo pamoja na uchangiaji wake ili kumpa mkulima unafuu.

3. **Bibi Zainab A. Chinowa (Katibu wa Chama cha Mapinduzi CCM (W)** alitoa pongezi nyingi kwa wajumbe kwa namna walivyoshiriki kikamilifu katika mkutano huo.

   Aliwashauri wawasaidie watendaji katika suala la udhibiti mapato ya Serikali hususani katika maeneo yao.

Vilevile alishauri ushirikiano uliopo kati ya wajumbe na watendaji uendelezwe ili kuweza kuwaletea wananchi maendeleo.

Vilevile aliwakumbusha watendaji kuendelea kuwasaidia wajumbe pale wanapohitaji usaidizi kutoka kwao.

Mwenyekiti (H/W) aliwashukuru viongozi kwa nasaha zao na kuahidi yote waliyoyaeleza yatazingatiwa.

**MUHT. NA.MDC 2020/2021: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa hajapokea mengineyo.

**MUHT. NA.MDC 2020/2021: KUFUNGA MKUTANO**

Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe, wageni waalikwa, watendaji na wadau wengine wote kwa namna walivyoshiriki kikamilifu katika mkutano huo.

Alisema kimsingi si kila maamuzi yanayotolewa yatamfurahisha kila mtu bali kinachozingatiwa ni kuona maamuzi hayo yanafanywa kwa maslahi ya wananchi.

Aligusia suala la ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kueleza kuwa anatumaini mapendekezo yote yaliyotolewa katika kuboresha ukusanyaji wa mapato hayo yatazingatiwa.

Mwisho alisisitiza ushirikiano uliopo uendelezwe ili kuwezesha kutekeleza majukumu mbalimbali kikamilifu kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo zaidi.

Alifunga mkutano mnamo saa 8.24 mchana.

**UMETHIBITISHWA NA:-**

| | |
|---|---|
| ......................................... | ......................................... |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |

05/08/2021
.........................
**TAREHE**